23 Juni 2022

**Leo ni Siku ya kumbukizi ya kuanzishwa kwa RITA**









# IJUE HISTORIA YA WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI (RITA)

Historia ya RITA inaanzia kabla ya Uhuru mnamo mwaka 1917 wakati Serikali ya Kikoloni ya Ujerumani ilipotunga Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo (Tangazo Na. 15 ya 1917 (Eneo la wananchi). Wakati Waingereza walipoichukua Tanganyika (Tanzania Bara) kutoka kwa Wajerumani waliutambua Utaratibu wa Usajili wa Vizazi na Vifo uliowekwa kwa Sheria za Kijerumani kwa kutambua daftari chini ya Sheria ya Usajili wa Vizazi na Vifo, 1920 (sura ya 108). Hata hivyo chini ya utawala wa mataifa yote mawili ya kikoloni usajili wa vizazi na vifo haukuwa wa lazima kwa Waafrika (Wazawa).

Kati ya mwaka 1920 na 1960 Serikali ya kikoloni ya Kiingereza ilianzisha Sheria kuhusu matukio muhimu ya maisha na masuala mengine. Sheria hizi ama zilisimamiwa kwa ujumla au kwa sehemu yake na Ofisi ya Kabidhi Wasii Mkuu/Msajili Mkuu. Mwaka 1961 Tanganyika ilipata Uhuru na Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba ilianzishwa. Miongoni mwa Idara za Wizara ilikuwa ni Idara ya Msajili Mkuu na Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu. Kila moja ya idara hizi ilikuwa na Sheria zake za kuzisimamia zikiwemo zile ambazo zinasimamiwa na RITA kwa sasa.

Kufuatia mabadiliko kadhaa ya Sera za Serikali hivyo kupelekea tamko la Azimio la Arusha, mwaka 1967 Wizara ya Sheria ilivunjwa na Idara mbalimbali zilizokuwa ndani ya Wizara hiyo zilihamishiwa kwenye Ofisi ya Makamu wa Rais na Waziri Mkuu kama Divisheni ambayo ilijulikana kama Divisheni ya Sheria.

Idara mbili za Kabidhi Wasii Mkuu na Msajili Mkuu ziliunganishwa kuwa idara moja iliyojulikana kama Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu. Wizara ilikuja kuundwa tena mwaka 1975 na mojawapo ya idara zake kuwa ile ya Kabidhi Wasii Mkuu.

Katika kuboresha Utumishi wa Umma chini ya Programu ya kuboresha Utumishi wa Umma (Public Service Reform Program), Serikali ilifikia uamuzi wa kuiboresha Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali, ambapo ndani yake kulikuwa na kitengo cha Msajili Mkuu kuwa Wakala wa Serikali. Lengo lilikuwa ni kuboresha huduma zitolewazo na Idara tajwa hapo juu, ili thamani ya hela ilingane na huduma inayotolewa.

Mchakato wa kuanzisha Wakala ulianza Februari 2003 na ilipofikia tarehe 23/6/2006 Wakala ulizinduliwa rasmi kwa jina la **WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI (REGISTRATION INSOLVENCY AND TRUSTEESHIP AGENCY (RITA).**

Uanzishwaji wa RITA umefanyika chini ya Sheria ya Wakala za Serikali Sura ya 245 (The Executive Agencies Act, Cap.245) na kutangazwa katika Gazeti la Serikali kwa Tangazo No. 397 la tarehe 12 Disemba 2005. Kazi zote zilizokuwa zikifanywa na Idara ya Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali zikiwemo za Usajili wa Vizazi na Vifo chini ya Msajili Mkuu sasa zinafanywa na RITA.

Mnamo mwaka 2018, maboresho yalifanyika tena kwa RITA kwa kupitia Sheria ya Kabidhi Wasii Mkuu (Mamlaka na Majukumu), Sura ya 27 ya mwaka 2018 ambayo ndiyo imeweka mamlaka ya utekelezaji wa majukumu yake.




Kabidhi Wasii Mkuu na Afisa Mtendaji Mkuu Bi. Angela Anatory (wa tatu kushoto), Naibu Kabidhi Wasii Mkuu Bi. Lina Msanga (wa pili kushoto) wakionesha keki maalum iliyoandaliwa kwa sehemu ya kuadhimisha miaka 16 tangu kuanzishwa kwa RITA mwaka 2006, wengine ni wawakilishi wa Wafanyakazi wa RITA.



TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa